JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI

**30 MEI, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI – 30 MEI, 2016

## I. KIAPO CHA UAMINIFU:

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
2. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
4. Mhe. Machano Othman Said
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA:**

Taarifa ya Mwaka ya Hesabu za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. *(The Annual Report and Accounts of Arusha International Conference Centre For The Year 2014/2015):*

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu baadhi ya Wabunge kufanya vurugu Bungeni na kudharau Mamlaka ya Spika tarehe 27 Januari, 2016.

## III. MASWALI:

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**257. MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu):- Suala la Makao Makuu ya Serikali kuhamia Dodoma kwa muda mrefu limekuwa na kigugumizi; na Ofisi za Wizara nyingi bado hazijahamia Dodoma kutokana na kutokuwepo Sheria inayotamka kuwa Dodoma ndio Makao Makuu ya Nchi:-

Je, ni lini Sheria hiyo itatungwa ili kuwezesha mchakato huo wa kuhamia Dodoma.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**258. MHESHIMIWA FELISTER ALOYCE BURA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kituo cha Afya cha Chamwino Ikulu kinahudumia zaidi ya Kata ishirini za Wilaya ya Chamwino; na wanawake na watoto wa Kata hizo wanategemea sana huduma za Kituo hicho lakini hakina vifaa tiba muhimu kama vile *Ultra sound*:-

Je, ni lini Serikali itanunua *Ultra sound* kwa ajili ya kituo hicho.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**259. MHESHIMIWA AUGUSTINE VUMA HOLLE (KASULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Pori la akiba la Kagera Nkunda lililoko Wilayani Kasulu lilianzishwa kipindi ambacho Wilaya ya Kasulu ilikuwa na wakazi wachache na kwa sasa idadi ya watu katika Wilaya hiyo imekuwa kubwa na kufanya mahitaji ya ardhi kuwa makubwa na hivyo kusababisha mgogoro baina ya Wakulima na Wafugaji na Mamlaka za Misitu na Wanyamapori:-

Je, Serikali imejipanga vipi kumaliza migogoro hii na kuwasaidia Wananchi.

## WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

### 260. MHESHIMIWA LEONIDAS TUTUBERT GAMA (SONGEA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Umeme ni muhimu sana kwa maisha bora ya Wananchi lakini Wananchi wa Songea Mjini hawana uhakika wa umeme kutokana na kutegemea zaidi umeme wa jenereta na ule kidogo unaozalishwa na Shirika la Masista wa Chipole:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa Gridi ya Taifa toka Njombe/Makambako;

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa watu wengi wanashindwa kuja kuwekeza Songea kutokana na kukosa umeme wa uhakika.

## WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

### 261. MHESHIMIWA KHATIB SAID HAJI (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Kwa mujibu wa Ibara ya 45 (1) (a) hadi (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano; Rais anayo mamlaka ya kutoa msamaha kwa wafungwa waliopo magerezani:-

Je, Rais anayo mamlaka kisheria ya kutoa msamaha kwa watuhumiwa wa uhalifu wa aina yeyote ambao mashauri yao yapo katika vyombo vya dola kwenye hatua za uchunguzi/ upelelezi au Mahakamani.

## WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

### 262. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Viwanja vya Ndege nchini ukiondoa Uwanja wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere Dar es Salaam havina miundombinu au huduma ya kubebea abiria wasiojiweza ikiwemo wagonjwa, wazee pamoja na watu wenye ulemavu:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa huduma hii katika viwanja vingine nchini;

(b) Huduma hii imekuwa ikifanya kazi na wakati mwingine kuharibika katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere Dar es Salaam; Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha huduma hii inapatikana muda wote kwenye Uwanja huu wa Mwalimu Nyerere.

**263. MHESHIMIWA HASSAN ELIAS MASALA (NACHINGWEA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani juu ya ujenzi wa barabara ya Masasi - Nanganga - Nachingwea yenye urefu wa km 91 kwa kiwango cha lami;

(b) Je, ni lini Serikali italipa fidia Wananchi wanaotakiwa kupisha ujenzi wa barabara hiyo hasa ikizingatiwa kuwa tathmini imeshafanyika muda mrefu.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**264. MHESHIMIWA CONCHESTER LEONCE RWAMLAZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Ni wajibu wa Serikali kulinda na kuhakikisha ustawi wa watoto katika nchi:-

Je, ni lini Serikali itatenga asilimia ya mapato yake katika bajeti ili kuwepo na mfuko wa kulinda ustawi wa watoto wa nchi hii.

**WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

**265. MHESHIMIWA PETER JOSEPH SERUKAMBA (KIGOMA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:-

Je, ni lini Serikali itajenga Soko la Kimataifa Kagunga mpakani mwa Tanzania na Burundi.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**(*Majadiliano yanaendelea*)**

## V. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE**

**DODOMA**
**30 MEI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**